**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA**
**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAMU (CMT) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA**
**TAREHE –22/04/2022**

**WATAALAMU WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Nassib B. Mmbagga | Mkurugenzi Mtendaji Wilaya | - Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Godhelp Ringo | -Afisa Utumishi Wilaya | - Katibu |
| 3. | Bw. Hoyange Mbwambo | -Afisa Kilimo Wilaya | |
| 4. | Bi. Magdalena Kimaro | -Mratibu wa TASAF Wilaya | |
| 5. | Bi. Zaina Mzindakaya | -Mweka Hazina Wilaya | |
| 6. | Bi. Fatuma Rajabu | -Katibu TSD Wilaya | |
| 7. | Dr. Flora Kessy | -Kaimu Mganga Mkuu Wilaya | |
| 8. | Bi. Vumilia Saimanga | -Mkaguzi wa ndani | |
| 9. | Bw. Lazaro Lemurua | -Afisa utumishi | |
| 10. | Bw. Msumari I.S. Msumari | - Afisa Misitu Wilaya | |
| 11. | Bw. Obadia R. Msemwa | -Afisa Nyuki Wilaya | |
| 12. | Bw. Mkumbo L.Ngoi | -Afisa TEHAMA Wilaya | |
| 13. | Bw. Nelson G. Mwankina | -Afisa Uchaguzi Wilaya | |
| 14. | Bi. Kiope Siwema Salum | -Afisa Habari Wilaya | |
| 15. | Bw. Temba Pascal | -Afisa Mipango Wilaya | |
| 16. | Bw. Ramadhani Mtinge | -Kaimu Mhandisi Ujenzi Wilaya | |
| 17. | Bw. Edward Mgaya | -Afisa Mifugo na Uvuvi Wilaya | |
| 18. | Bw. Johari Mtango | -Afisa Mtendaji Mamlaka Mji Mdogo Muheza | |
| 19. | Bi. Herieth Nyangasa | -Mratibu wa kuthibiti UKIMWI Wilaya | |
| 20. | Bi. Vije Ndwanga | -Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya | |
| 21. | Bi. Desderia Haule | -KatibuTawala Wilaya | |
| 22. | Bw. Cyprian Mselemu | -Afisa Mazingira Wilaya | |
| 23. | Bw. Thomas E. Mkwavi | -KaimuAfisa Ardhi Wilaya | |
| 24. | Bw. Moses Mpembo | -KaimuAfisaMapato Wilaya | |
| 25. | Bi. Pilly Maximillian | -Afisa Elimu Msingi Wilaya | |
| 26. | Mwl. JuliethJ. Haule | -MdhibitiUborawa Elimu yaMsingi Wilaya | |
| 27. | Bw. Serapion Bashange | -Afisa Elimu Sekondari Wilaya | |
| 28. | Bi. Aisha Mhando | -MwanasheriawaHalmashauri | |
| 29. | Bw. Ngulizi Julius | -Mwanasheria | |
| 30. | Bw. Gregory Shangai | -Afisa Biashara Wilaya | |

**WAANDISHI:**
1. Bw. Gerald Gweba.
2. Bi. Zaituni Saidi

**12/2021/2022/121:** **KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 03:30 asubuhi.

**12/2021/2022/122:** **KUTHIBITISHA AJENDA ZA KIKAO.**

Katibu aliwasilisha ajenda za kikao na wajumbe walizikubali kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha ajenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha kamati ya wataalamu tarehe 23/03/2022.
4. Utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha wataalamu tarehe 23/03/2022.
5. Taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri mwezi Machi 2022.
6. Taarifa ya mapato ya mfuko wa afya ya jamii CHF, ICHF, Papo kwa Papo na Bima ya Afya ya Taifa NHIF kwa mwezi Machi 2022.
7. Taarifa ya marejesho ya Mikopo vikundi vya wanawake, vijana na walemavu Machi, 2022.
8. Taarifa ya ziara ya ukaguzi wa miradi robo ya tatu 2022.
9. Taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo robo ya tatu 2022.
10. Taarifa ya manunuzi ya Halmashauri robo ya tatu 2022.
11. Taarifa ya kamati ya ukaguzi robo ya tatu 2022.
12. Mapendekezo ya mfanyakazi hodari mwaka 2022
13. Sheria ndogo za Halmashauri 2022.
14. Maombi ya kutangaza zabuni 2022/2023.
15. Kufunga kikao.

**12/2021/2022/123:** **KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAMU CHA TAREHE 23/03/2022.**

Muhutasari wa kikao cha kamati ya wataalamu cha tarehe 23/03/2022 ulisomwa na wajumbe wote na baadae mwenyekiti na katibu waliweka saini kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu halali ya kikao hicho.

**12/2021/2022/124:** **UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 22/04/2022.**

**a) MAOMBI YA FEDHA SH. 109,888,867/= KUENDELEZA KITUO CHA AFYA KWAFUNGO.**

I. Mchanganuo wa matumizi ya fedha uhakikiwe na taarifa iwasilishwe Kikao kijacho baada ya uhakiki.

**b) TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI MWEZI MACHI, 2021.**

I. Afisa Mifugo afuatilie kwa makini idadi ya mifugo inayochinjwa na kuwa na takwimu zitakazoendana na mapato yanayopatikana. Taarifa iwasilishwe kikao kijacho.

II. Afisa Mazingira afuatiliaji kuhusu mapato yanayopatikana na machimbo ya mawe, mchanga na kokoto na taarifa iwasilishwe kikoa kijacho.

III. Afisa mipango afuatilie kuhusu Mtambo wa maji na Taarifa itolewe kikao kijacho.

IV. Afisa Ardhi afuatilie vibanda vilivyopo eneo la kanisa na taarifa iwasilishwe kikao kijacho

**c) TAARIFA YA ZIARA YA UKAGUZI WA MIRADI ROBO YA TATU 2022.**

I. Mkaguzi wa ndani akague miradi iliyopo Mgoda, Kwabada, Mkuzi na Tongwe na taarifa iwasilishwe kikao kijacho.

**12/2021/2022/125: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI MWEZI MACHI, 2022**

Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya Halmashauri kwa Mwezi Machi, 2022. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote. Kwa muhutasari taarifa hiyo ni kama ifuatayo

**MAPATO:**

Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Halmashauri ya wilaya ya Muheza imekisia kukusanya jumla ya Sh **36,471,098,539.00** kutoka kwenye vyanzo vyake vyote vya mapato. Hadi mwezi March, 2022 Halmashauri imekusanya mapato ya ndani, ruzuku, na miradi ya maendeleo ya jumla ya **Sh 23,337,781,136 s**awa na 64**%** ya makisio.

| Chanzo cha Mapato | Makisio 2021/2022 | Jumla ya Mapato halisi Julai - Feb 2022 | Mapato halisi March, 2022 | Jumla ya Mapato Julai - March 2022 | Asilimia % |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2,130,000,000 | 1,635,340,217 | 309,578,476 | 1,944,918,693 | 91% |
| CHF,NHIF, Ada(Afya ya Jamii) | 180,000,000 | 99,426,420 | 29,049,248 | 128,475,668 | 71% |
| Ada za sekondari | 119,400,000 | 97,068,877 | 18,381,100 | 115,449,977 | 97% |
| Ada ya Taka | 20,412,000 | 11,870,500 | 0 | 11,870,500 | 58% |
| Ruzuku Mengineyo | 779,075,000 | 684,167,170 | 50,118,416 | 734,285,586 | 94% |
| Ruzuku Mishahara | 23,046,673,000 | 13,372,929,280 | 1,891,514,000 | 15,264,443,280 | 66% |
| Ruzuku miradi ya Maendeleo | 10,195,538,539 | 4,569,388,486 | 568,948,946 | 5,138,337,432 | 50% |
| | **36,471,098,539** | **20,470,190,949** | **2,867,590,186** | **23,337,781,136** | 64% |

**MATUMIZI:**
Hadi kufikia mwezi March, 2022, Halmashauri ya wilaya ya Muheza imetumia jumla ya Sh **22,639,666,623.63** sawa na 62**%** ya bajeti ya 2021/2022.

| **Chanzo cha Mapato** | **Makisio 2020/2021** | **Jumla ya Matumizi Julai-Feb 2022** | **Matumizi Halisi March 2022** | **Jumla ya Matumizi Julai-March 2022** | **Asilimia %** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya Ndani | 2,130,000,000 | 1,341,130,684 | 70,151,593 | 1,411,282,277 | 66% |
| CHF(Afya ya Jamii) | 180,000,000 | 45,604,622 | 7,991,169 | 53,595,791 | 30% |
| Ada za sekondari | 119,400,000 | 62,974,523 | 19,188,137 | 82,162,660 | 69% |
| Ada ya Taka | 20,412,000 | 10,564,745 | 0 | 10,564,745 | 52% |
| Ruzuku Mengineyo | 779,075,000 | 360,277,223 | 43,133,800 | 403,411,023 | 52% |
| Ruzuku Mishahara | 23,046,673,000 | 13,375,860,595 | 1,891,514,000 | 15,267,374,595 | 66% |
| Ruzuku miradi ya Maendeleo | 10,195,538,539 | 4,466,062,958 | 945,212,575 | 5,411,275,533 | 53% |
| **JUMLA** | **36,471,098,539** | **19,757,220,850.54** | **2,977,191,274.09** | **22,639,666,623.63** | **62%** |

## USULUHISHI WA KIBENKI ( RECONCILIATION)

Mpaka kufikia mwezi March usuluhishi wa akaunti saba za Halmashauri zilizopo BOT ( Education Sector Acc, Health Sector Acc, other Charge Acc, Peronal Emolument Acc,Reccurrent Ownsource Acc, Development Ownsource Acc, na Development Exchequer Acc), akaunti tatu ambazo zipo katika benki za biashara ( Commercial Banks): Miscellaneous Deposit, Muheza Dc Ownsource Revenue Collection na WYDT Acc, usuluhishi unaendelea.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa.

## 12/2021/2022/126: TAARIFA YA MAPATO YA MFUKO WA AFYA YA JAMII CHF, ICHF, PAPO KWA PAPO NA BIMA YA AFYA YA TAIFA (NHIF) KWA MWEZI MACHI, 2022.

Mganga mkuu aliwasilisha taarifa ya mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii CHF, ICHF, Papo kwa papo na Bima ya Afya (NHIF) kwa mwezi Machi, 2022. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote, kwa muhtasari taarifa hiyo ni kama ifuatavyo:-

Kwa kipindi cha mwezi Machi 2022, Jumla ya **Tshs. 9,864,950/=** zimekusanywa kutokana na michango ya papo kwa papo**, Tsh.13, 503,640/=** zimekusanywa kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na **Tsh.5, 680,658/=** zimekusanywa kutoka Mfuko wa Afya ya Jamii ilioboreshwa (ICHF).Jumla kuu ni **Tsh.29,049,248/=**

Aidha tangu kuzinduliwa kwa CHF Iliyoboreshwa tarehe 10/10/2019 jumla ya kaya **2126** zimejiunga sawa na asilimia **15.7** ya kaya lengwa **13,560** ifikapo Juni 2022

Kwa kipindi cha Mwezi Machi 2022 vituo vya kutolea huduma za Afya vimetoa huduma kwa makundi ya msamaha zenye thamani ya **Tsh.47,745,558/=** ambapo Gharama za Kumuona daktari **24,768,000/= (51.87%),** Vipimo na Dawa **Tsh.22,977,558/= (48.13%).**

**MIKAKATI YA KUFIKIA LENGO LA UANDIKISHAJI WA ICHF**

1. Kufanya ufuatiliaji wa malipo ya ICHF kutoka Mkoani ili kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa kwa wateja wa ICHF

2. Kuendelea kufanya uhamashishaji wa ICHF kupitia mikutano ya hadhara, shule, vikundi vya ujasiriamali, Walegwa wa Tasaf na vikundi vya Boda Boda

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, mipango kujadiliwa

**12/2021/2022/127: TAARIFA YA MAREJESHO YA MIKOPO VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU MACHI, 2022.**

Afisa maendeleo ya jamiialiwasilisha taarifa ya  taarifa ya marejesho ya mikopo vikundi vya wanawake, vijana na walemavu machi, 2022. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote, kwa muhtasari taarifa hiyo ni kama ifuatavyo

Kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 Halmashauri imetenga Tshs 213,000,000/= kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi 42 vya uzalishaji mali vya wanawake, vijana na Watu wenye walemavu.

Kwa kipindi cha Machi 2021/2022, Halmashauri imetoa mikopo yenye thamani ya Tsh. 100,000,000/= kati ya fedha hizo Mapato ya ndani Tshs 50,000,000/= na marejesho 50,000,000/= kwa ajili ya kukopesha vikundi 14 vyenye jumla ya washiriki 80, vikiwemo vikundi vya wanawake 7 vyenye wanufaika 47 vimekopeshwa Tshs.45,000,000/=, vijana 5 vyenye wanufaika 26 vimekopoeshwa Tshs. 45,000,000/=  na watu wenye ulemavu 2 vyenye wanufaika 7 vimekopeshwa Tshs. 10,000,000/=

**HALI HALISI YA MAREJESHO NA MADENI YA MIKOPO YA VIKUNDI KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI -2022 KWA VIKUNDI VYA MWAKA 2010-2022**

Kwa kipindi cha Mwezi Machi - 2022 Jumla ya Tshs. **26,574,700 /=** zimerejeshwa kutoka vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mchanganuo ufuatao:-

- **Marejesho kwa vikundi vilivyokopeshwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

Vikundi vya wanawake Tshs. 4,884,000.00

Vikundi vya Vijana Tshs. 6,129,000.00

Vikudi vya Walemavu Tshs. 1,200,000.00

**JUMLA Tshs. 12,213,000.00**

- **Marejesho kwa vikundi vilivyokopeshwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

Vikundi vya wanawake Tshs. 6,746,000.00

Vikundi vya Vijana Tshs. 6,555,700.00

Vikudi vya Walemavu Tshs. 570,000.00

**JUMLA Tshs. 13,871,700.00**

- **Marejesho kwa vikundi vilivyokopeshwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

Vikundi vya wanawake Tshs. 350,000/=

Vikundi vya Vijana Tshs. 0

Vikudi vya Walemavu Tshs. 0

**JUMLA Tshs. 350,000 /=**

- **Marejesho kwa vikundi vilivyokopeshwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019**

Vikundi vya wanawake Tshs. 100,000/=

Vikundi vya Vijana Tshs.400,000/=

Vikudi vya Walemavu Tshs. 0

**JUMLA Tshs. 140,000/=**

- **Marejesho kwa vikundi vilivyokopeshwa mkopo kwa mwaka wa fedha 2010 hadi 2018**

Vikundi vya wanawake Tshs. 0

Vikundi vya Vijana Tshs. 0

**JUMLA Tshs. 0/=**

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa

**12/2021/2022/128: TAARIFA YA UTEKELEZAJI MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU 2022.**

Katibu Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya utekelezaji miradi ya maendeleo robo ya tatu Januari hadi Machi 2022, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote, kwa muhtasari taarifa hiyo ni kama ifuatavyo

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Muheza inatarajia kufanya matumizi kwenye miradi ya maendeleo kiasi cha Shs 11,399,175,676. Ambapo fedha kiasi cha Shilingi 852,000,000.00 ni mapato ya ndani. Aidha, Halmashauri imepokea shs 10,120,566,254 ikiwemo na fedha Shs 2,541,589,865 na fedha zilizovuka mwaka 2020/2021.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa. (Kiambatanisho kimeambatanishwa)

**12/2021/2022/129: TAARIFA YA MANUNUZI YA HALMASHAURI ROBO YA TATU 2022.**

Afisa manunuzi aliwasilisha taarifa ya manunuzi robo ya tatu Januari hadi Machi 2022, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote, kwa muhtasari taarifa hiyo ni kama ifuatavyo

Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imefanya manunuzi yenye thamani ya Tsh. 172,154,495.04/= kwa mchanganuo ufuatao

| | |
|---|---|
| • Vifaa | 153,229,635.04/= |
| • Huduma zisizo za kitaalam | 18,924,860/= |
| • Huduma za kitaalam | - |
| • Kazi | - |
| **JUMLA** | **172,154,495.04/=** |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa.

**12/2021/2022/130: TAARIFA YA KAMATI YA UKAGUZI ROBO YA TATU JANUARI-MACHI, 2021/2022**

Mkaguzi wa ndani aliwasilisha taarifa ya kamati ya ukaguzi robo ya tatu Januari-Machi, 2021/2022, nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote, kwa muhtasari taarifa hiyo ni kama ifuatavyo

Katika kipindi cha Robo ya pili Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Fedha na Biashara (Mapato na matumizi), Utumishi na Utawala, Manunuzi, TASAF III, Elimu Msingi na Sekondari,

Maendeleo ya Jamii, na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita ya Mkaguzi wa Ndani na Mkaguzi wa Nje.

Katika kipindi cha Robo ya pili (Oktoba – Desemba, 2021), Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kimefanya mapitio ya majibu ya hoja 18 za vipindi vilivyopita, hoja 7 zimefungwa na kubakia na hoja 11 zinazosubiri utekelezaji katika robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Pia katika kipindi cha robo ya pili, Oktoba hadi Desemba,2021 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mkaguzi ametoa hoja 8 ambazo bado zinaendelea kufanyiwa utekelezaji na Idara husika, hivyo kufanya kuwa na jumla ya hoja 19 zinazosubiri utekelezaji kutoka kwa Wataalamu.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa

**12/2021/2022/131: MAPENDEKEZO YA WATUMISHI HODARI KWA MWAKA 2020/2021 HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA.**

Afisa utumishi aliwasilisha taarifa mapendekezo ya watumishi hodari wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa mwaka 2021/2022 orodha ya watumishi waliopendekezwa iligwiwa kwa wajumbe wote. Kwa muhtasari mapendekezo hayo ni kama yafuatayo.

Idara kwa kushirikiana na vyama vya wafanyakazi imekamilisha zoezi la kuwapata wafanyakazi hodari na inapendekeza watumishi hawa wapewe zawadi ya shilingi 100,000/= kila mmoja kwa kuzingatia bajeti iliyotengwa

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa

**12/2021/2022/132:MAPENDEKEZO YA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI ZA MWAKA 2022.**

Mwanasheria aliwasilisha taarifa mapendekezo ya sheria ndogo. Nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe wote na kwa muhutasari ni kama ifuatavyo.kama yafuatayo

Halmashauri ina mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo na inatarajia kutunga Sheria Ndogo ambazo zitasaidia katika ukusanyaji wa mapato katika eneo la mamlaka yake. Sheria ndogo hizo zimetungwa kufuatia matakwa ya kifungu cha 7 cha Sheria za fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 ya Sheria za Tanzania na kifungu cha 153 cha Sheria za Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287 ya Sheria za Tanzania.

Kwa mamlaka iliyopewa na sheria hizo Halmashauri inakusudia kutunga sheria ndogo 2 na kufanya marekebisho kwa sheria ndogo nyingine 5 kama inavyoonekana kwenye taarifa hii. MAPENDEKEZO ya viwango vilivyoainishwa

kwenye sheria ndogo hizi zimewasilishwa kwa wadau hususan watendaji wa Kata zote ili Kamati za Maendeleo za Kata zitoe maoni yao ili zilwasilishwe kwenye Mamlaka kwaajili ya idhini.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa

**12/2021/2022/133: MAOMBI YA KUTANGAZA ZABUNI 2022/2023**

Afisa manunuzi aliwasilisha maombi ya kutangaza zabuni 2022/2023 nakala ya taarifa hiyo waligawiwa wajumbe na taarifa ilikuwa kama ifuatavyo.

Halmashauri inawasilisha Maombi ya idhini ya kutangaza zabuni mbalimbali za wakala wa ukusanyaji ushuru kama ifuatavyo.

I. Wakala wa ushuru wa mazao isipokuwa korosho, mkonge na masambu.
II. Wakala wa ushuru wa mchanga, mawe na kokoto.
III. Wakala wa ushuru wa vyoo vya soko la michungwani na stendi ya Bomani.
IV. Wakala wa ushuru tozo za usafirishaji mji.
V. Wakala wa ulinzi

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kukubaliana iende kamati ya fedha, uongozi na mipango kujadiliwa

**12/2021/2022/134:** **KUFUNGA KIKAO.**
Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa usikivu wakati wote wa kikao alifunga kikao saa 08:30 mchana.

**UMETHIBITISHWA:**

..............................
**KATIBU**

**TAREHE:** 17/5/2022

..............................
**MWENYEKITI**

KIAMBATA C

| TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA FEDHA ZA UVIKO - 19 (TCRP 5441). | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NA | LENGO LA MWAKA | UTEKELEZAJI | | FEDHA | | | MAELEZO |
| | | MAUMBILE | % | TENGWA | TOLEWA | TUMIKA | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 1 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Bwembwera | darasa 1 limekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 2 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa katika shule Sekondari Chief Mang'enya | Ujenzi umekamilika | 100 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 3 | Ujenzi wa Chumba 1 vya darasa katika shule Sekondari Kerenge | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 4 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Kicheba | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 5 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Kigombe | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 6 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa katika shule Sekondari Kilulu | Ujenzi umekamilika | 100 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 7 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa katika shule Sekondari Majengo | Ujenzi umekamilika | 100 | 80,000,000 | 80,000,000 | 80,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 8 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Kwabutu | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 9 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Mpapayu | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 10 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa katika shule Sekondari Kwafungo | Ujenzi umekamilika | 100 | 80,000,000 | 80,000,000 | 80,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 11 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa katika shule Sekondari Kwemkabala | Ujenzi umekamilika | 100 | 80,000,000 | 80,000,000 | 80,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 12 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Magila | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 13 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa katika shule Sekondari Misalai | Ujenzi umekamilika | 100 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 14 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Misozwe | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 15 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Mkurumuzi | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 16 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Mkuzi | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 17 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Mlinga | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 18 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Mlingano | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |

| NA | LENGO LA MWAKA | UTEKELEZAJI | | FEDHA | | | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MAUMBILE | % | TENGWA | TOLEWA | TUMIKA | |
| 19 | Ujenzi wa vyumba 1 vya madarasa katika shule Sekondari Mtindiro | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 20 | Ujenzi wa vyumba 2vya madarasa katika shule Sekondari Kwabada | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 21 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Ngomeni | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 22 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Nkumba | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 23 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule ya Sekondari Tongwe | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 24 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Zigi | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 25 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Potwe | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 26 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa katika shule Sekondari Shebomeza | Ujenzi umekamilika | 100 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 27 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa katika shule Sekondari Songa | Ujenzi umekamilika | 100 | 80,000,000 | 80,000,000 | 80,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 28 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa katika shule Sekondari Zirai | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 29 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa kwenye vituo Shikizi shule za Msingi Bebere | Ujenzi umekamilika | 100 | 80,000,000 | 80,000,000 | 80,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 30 | Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa kwenye vituo Shikizi shule za Msingi Kwemkabala | Ujenzi umekamilika | 100 | 80,000,000 | 80,000,000 | 80,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 31 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shikizi shule za Msingi Jambe | Ujenzi umekamilika | 100 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| 32 | Ujenzi wa Bweni 1 Shule ya Msingi yenye mahitaji maalum shule ya msingi Ngomeni | Jengo limepauliwa na kuwekwa grili za madirisha | 75 | 80,000,000 | 80,000,000 | 80,000,000 | Fedha zimekwisha. Taratibu za kuomba fedha hazina zinaendelea |
| 33 | Ujenzi wa nyumba ya daktari (3 in one) | Jengo limekamilika | 80 | 90,000,000 | 90,000,000 | 90,000,000 | Ujenzi Umekamilika |
| **JUMLA YA FEDHA ZA UVIKO - 19 (TCRP 5441).** | | | | **1,510,000,000** | **1,510,000,000** | **1,510,000,000** | |
| | | | | | | | |